



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: 0232935443
Nukushi: 0232935442
Baruapepe:td@nanyambatc.go.tz

2 Barabara ya Bomani,
S.L.P 1490,
63682 NANYAMBA-MTWARA

Tafadhali taja:

Kumb. Na. NTC/89/345/0/VOL III/62

Tarehe 21/09/2024

**TANGAZO LA KAZI YA UANDIKISHAJI WAPIGA KURA KWA UCHAGUZI WA
SERIKALI ZA MITAA 2024**

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Mji Nanyamba anawatangazia Watumishi wa Umma wote nafasi za kazi kwa ajili ya Shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika siku ya Jumatano tarehe 27/11/2024.

1.0 NAFASI ZINAZOTANGAZWA

MWANDIKISHAJI WAPIGA KURA - NAFASI 333

2.0 SIFA ZINAZOTAKIWA

- i. Awe Raia wa Tanzania.
- ii. Awe ni Mtumishi katika Utumishi wa Umma
- iii. Asiwe na dhamana au uongozi katika chama chochote cha siasa
- iv. Awe Mwadilifu

3.0 JINSI YA KUOMBA

- i. Barua ya mwombaji iandikwe kwa mkono
- ii. Barua iandikwe majina kamili yanayotumika katika Utumishi
- iii. Barua itaje nafasi ya kazi unayoomba
- iv. Barua itaje cheo katika Utumishi wa Umma
- v. Barua itaje kituo cha kazi
- vi. Barua iwe na anwani kamili na namba ya simu inayopatikana wakati wote
- vii. Barua iambatanishwe na maelezo binafsi (CV)
- viii. Barua ziwasilishwe Masijala ya Wazi Ofisi ya Halmashauri kupitia anuani ifuatayo;

Msimamizi wa Uchaguzi,
Halmashauri ya Mji Nanyamba,
S.L.P 1490,
NANYAMBA.

Tarehe ya kuomba ni kuanzia tarehe 21/09/2024 hadi tarehe 27/09/2024 saa 9:30 Alasili.


Eng. Mshamu A. Munde
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
NANYAMBA

